***POOZA***

**NENO**

Siku ya sabato alikuwa akifundisha katika sinagogi mojawapo. Na tazama palikuwa na mwanamke aliyekuwa na pepo wa udhaifu muda wa miaka kumi na minane naye amepindana hawezi kujinyoosha kabisa (Luka 13:10-11)

Fikiri kila fungu la maneno katika mistari hii na orodhesha yaliotendeka. Orodhesha uliyoyagundua uliyoyaona na uliyoyatambua.

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________
4. ______________________________
5. ______________________________
6. ______________________________
7. ______________________________
8. ______________________________

Sasa simulia tena habari hii kwa kutumia maneno yako ya karne hii ya 21.

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

MASWALI Kuhusu HABARI

1. Nini umuhimu wa tukio hili?
2. Nani wahusika wakuu.
3. Nini tatizo.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**MASWALI YA KUTAFAKARI.**

1. Ni kwa namana gani najigundua mwenyewe kujilinganisha na mwamake aliyepooza?
2. Ni mawazo gani na mtazamo upi unakusukuma kupooza?
3. Ni watu gani ambao maneno yao na matendo yao yamesababisha mgongo wako kupooza?
4. Ni uzoefu (mapito) gani umekusababishia aibu masumbuko au udhaifu wa mwili.

**WAKATI WA KUJIHOJI**

Fikiri juu ya habari ruhusu neno la Mungu lipenye moyoni mwako sikiliza Bwana anayokupa mameno ya faraja na tumaini. Jiachia kuandika mawazo mbalimbali jinsi yanavyokuja katika fahamu zako. Andika sentensi au aya lakini anza kwa hatua ya kuweka mawazo yako katika maneno. Waweza kuamua kununua kijitabu cha kuandika.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

**MUDA WA SALA**

Baba wa mbinguni umeniumba mimi –mwili ufahamu na roho. Hamu yako ni kwamba niishi maisha ya kuinuliwa juu ya kusimama imara katika pendo lako, pendo ambalo ni langu kwa sababu ya dhabibu ya mwanao. Kama mwamamke katika habari mimi pia nimepooza. Hali yangu hii ni sehemu yangu ambayo sijitambui kwa kiasi gani kweli nilivyopooza. Leo Bwana nimeanza kutambua kwamba nimevunjika nimejeruhiwa na nimeumizwa na historia yangu ya nyuma. Nipe ujasiri kujiamini mwenyewe.

Nitie nguvu kujiachia na kukiri mambo yaliyonifanya nipooze. Kwa sababu ya Yesu ameniweka huru.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Baba umeniumba kwa hofu na kwa ajabu siku ya leo nazingatia mahusiano, uzoefu na hatia zimenifanya kupooza mimi mwenyewe nazingatia mambo ya maisha yangu ya kimwili, kiakili na kiroho-nazingatia watu na matukio ya sasa na ya zamani nayaleta mbele yako…

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

**MAMBO YA KUFANYA KILA SIKU**

Kutokana na habari hii toka biblia na kujihoji juu ya jinsi maisha yangu yanavyohusiana na mwamake aliyepooza ni watu gani watafu ninao wafahamu ambao wanateseka na hali yao ya kupooza? Wiki hii nitaomba kwa ajili ya:

1. ________________________________________
2. ________________________________________
3. ________________________________________

Sala yangu ni hii

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________


©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**ITWA**

**NENO**

Yesu alipomwona alimwita (Luke 13:12a).

Yaliyotendeka hapa ni mafupi na rahisi

1. ______________________________________________
2. ______________________________________________

**MASWALI NA MAONI KUHUSU HABARI**.

1. Yesu alikuwa akifundisha katika sinagogi, ni sehemu ya wayahudi ya ibada na kujifunza. Itakuwaje ukigundulika na mtu fulani mwalimu au yeyote akuite kwa jina lako hadharani?

2. Itakuwaje kufikiri hukugundulika na huonekani uko mahali gani na ghafla inakuwa mtu wa kutazamwa na kila mmoja? Yesu alimwita mwanamke aliyepooza jina lake (Daktari atakuona wewe sasa).

Yesu alimwita hakuwa na nafasi ya kutengeneza nywele zake kujiremba au kujingalia. Alichofahamu ni kwamba jina lake limeitwa na alikua mtu peke kuitika kwa hiyo alinuka toka kitini mwaka akaanza kutembea kuelekea kwa Yesu.

Kuna mtu aliyemwita mwanamke huyu toka sehemu yake maficho na kumfanya mtu maalum hakuweza kutomjali na kumwachilia mbali. Hakumfanyia mzaha au kutoa mawazo ya dharau juu ya umbo lake la kupindana badala yake Yesu alimwita kama alivyo mpenda Yesu alimwangalia kwa huruma na akamwita kwa jina lake!

Jifanye kuwa mwamke aliyepooza kwenye sinagogi siku ile. Ulikuwa ukisikiliza jinsi Yesu alivyokuwa akifundisha na ghafla Yesu kasimama na kuita jina lako onyesha msisimko wako na woga hisia na tumaini lako "Daktari atakuona *wewe* hali sasa."

**MASWALI YA KUTAFAKARI**

1. Jina langu ni ________________________________ Je nalipenda Jina langu?
   (Ma) Jina langu la utani ni __________________________Najisikiaje kuhusu (Ma) JINA (haya) hili?

2. Fikiri ni mahali gani jina lako linapoitwa unajisikiaje mahali mbalimbali inapokuwa na watu tofauti?
3. Yohana 10:3 inasema "naye hawaita kondoo wake kwa majina yao,…" Ina maana gani kwako unaposikia Yesu anakuita wewe kwa jina lako?

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

4. Mungu ametoa thamani kubwa na mamlaka juu ya jina lake mwenyewe. Amri yake ya pili (Kutoka 2:7) inatufundisha jinsi ya kuliheshimu Jina Lake. Nguvu na mamlaka nimetolewa katika Jina la yeyote. Kama watoto wawili wanagombana kwa hali isiyoepukika mtu aweza kukimbia kwa mama na kurudi na maneno ya nguvu na mamlaka "Mama anasema…" ni wakati gani jina lako limekashifiwa umekuwa katika hatari au mtu amelitumia vibaya? Ni watu/Mtu gani hao huyo anahusika?

**WAKATI WA KUJIHOJI**.

Kama mwamake aliyepooza ninapambana na hali yangu ya kupooza ye kutokuwa na imani mambo mengi yananifanya kufungwa –historia yangu mahusiano yangu mtazamo/mwelekeo wangu ratiba yangu hatia yangu tabia mbaya. Lakini leo mshale wa matumaini unaniangaza moyoni mwangu. Yesu ameniita mbele Tumaini li katika sauti Yake. Huruma imo machoni mwake. Ameniita amenitenga kama anavyosikiliza katika moyo wangu ninavyojisikia.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**WAKATI WA SALA**

Oh Yesu umeniita kwa jina unanifahamu unanijua nilivyo na yote yanihusuyo unayafahamu yaliyonikaribu na kunifanya nimefungwa unajua hatia na aibu ninayobeba unafahamu uzoefu wangu wa kale na jinsi ulivyoniharibu umbile langu sifa zangu, utu wangu, mwelekeo wangu.

Bado licha ya kufahamu yanayonihusu umenithamini umekataa kuiruhusu hali yangu kuharibu uhusiana wetu upendo wako unaiita kuja kwako. Wito wako wa upnendo unaniambia kwamba mimi ni wa thamani na naweza kuja kwako jinsi nilivyo. Wito wako wasema hakuna kitakachotutenga nawe kwa kuwa hamu yako ni kwamba wote waje katika mahusinano ya wokovu pamoja nawe. Wito wako ni wito wa kweli. Ndio, Yesu unanipenda. Hivi ndivyo nijuavyo.

Leo nataka kusema asante. Asante kwa kuniita mbele. Asante kwa kunipenda. Asante kwa kuniona kwamba naishi na kwamba mimi ni mtu uliyenijaza fikra na hisia Asante kwa…

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**MAMBO YA KUFANYA KILA SIKU**

Nikizingatia wale ambao nimekuwa nikiwaombea kwa siku hizi, ni jinsi gani natumia majina yao kwa njia ya kuwaheshimu na kuwainua kama Yesu alivyofanya kwa mwanamke aliyepooza alipomwita mbele? Kipindi kijacho (wakati mwingine) ___________________ Nitawasiliana na kila mmoja ambaye nimekuwa nikimwinua kwa sala. Nitahitaji kuwaheshimu na kuwathamini kwa…

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**SAMEHEWE**

**NENO**

[Yesu] akamwambia "Mama Umefunguliwa katika udhaifu wako" (Luka 13:12)

Tena mambo yaliyotendeka ni mafupi na rahisi

1. ________________________________________
2. ________________________________________

Mwandishi wa Injili Mtakatifu Yohana anamwita YESU

"Neno akafanyika mwili" Neno huongea Neno

"Mama umefunguliwa katika udhaifu wako"

**MASWALI NA MAONI KUHUSU HABARI**.

1. Mwanamke aliyepooza alikuwa na hadhara na Yesu mwenyewe, Mwokozi wa ulimwengu. Huyu Yesu alikuwa nani? Unafahamu nini kuhusu Yeye? Fikiri juu ya kuwa unajua nini kuhusu Yeye [Yesu] na zingatia chimbuko la taarifa yako.

2. "Umefunguliwa" Mwanamke alikuwa amefungwa kwa miaka kumi na nane Yesu amemfungua! Lakini kitu gani kilimfanya afungwe? Kutoka katika nini Yesu amemfungua? Ni roho ya namna gani iliyomfanya apooze? Ulikuwa mzigo gani wa utumwa ambao Yesu alimfungua?

3. Yesu ametambua tatizo la ndani –tatizo ambalo lilikuwa asili ya ulemavu wa mwili. Sio tu kwamba inavuta Yesu anaposema "Umefunguliwa" sio kwamba ingekuwa kawaida Yesu kusema vinginevyo kama "Mwanamke tembea wima kwa kunyooka" laikini kwa kweli kifungo chake kimo mwetu sisi sote. Kifungo chake kama vyetu ni dhambi na mzigo mzito wa hatia tunaobeba.

Mambo yanayohusiana na roho ni ya muhimu kwa Yesu. Yesu aweza kuona ulemavu wa mwili wa manamke lakini zaidi ya yote alitaka kumfungua toka dhambi na hatia ambavyo vilimsababisha kutokuwa na uhusiano na Baba wa mbinguni. Alifahamu udhaifu wake [mwanamke].

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Aliweza kuona amepooza toka maisha ya kawaida na yamemtesa.  Lakini juu ya hayo yote alifahamu uzito wa hatia iliyogusa sio mwili wake tu bali na roho yake.  Maneno [Mwanamke] “umefunguliwa” yalikuwa maneno ya uzima, ya tumaini, ya upendo.

**MASWALI YA KUTAFAKARI**

1. Andika mstari wa leo, weak jina lako kwenye neno “Mwanamke”.

2. Neno limeshasemwa Yesu anasema “Umefunguliwa” mzigo gani unaokulemea unaoubeba mabegani mwako?  Kwa mambo gani uliyoyafanya ambayo unakataa kusamehe mwenyewe?  Nani hao ambao wametenda dhambi dhidi yako ambo unaona ni vigumu kusamehe?

3. Fikiri Yesu anachukua udhaifu na anauinua mzigo uliolemea mgongo katika mabega yako na anakufungua.  Anachukua uzito wa mzigo wako katika mabega yake.  Mwache Yesu achukue mzigo wako wa dhambi na hatia.  Ameshaubeba tayari kwa ajili yako msalabani.  Maisha yake, kifo, no kufufuka knwake kumekufungua wewe.

**WAKATI WA KUJIHOJI**.

Sikiliza kwa utulivu Bwana anavyosema maneno Yake ya upendo na msamaha kwako kupitia Neno Lake.  Pokea uhuru anaokupa “Basi Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli? (Yohana 8:36)  Andika maneno yako ndani ya Kristo Yesu yanayoelezea uhuru huu.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**WAKATI WA SALA**

Oh Bwana, kama mwanamke aliyepooza, mimi pia naja kwako nikitubu dhambi na hatia zinazonikandamiza chini.  Nabeba udhaifu wa hatia, naendelea kuzingatia mambo ya mwisho ambayo sikuyakosea, nikiikataa hasira na chuki ninayoisikia kwa watu walionitendea mabaya. Najitoa kwamba sina hasira, natubu dhambi na hatia ninazobeba Zimekuwa sehemu yangu kwa mda mrefu naweza kulia kwako [Bwana] kwa ajili ya.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Upendo na msamaha kwa ajili ya huruma na neema ambavyo vyatokana na imani pekee ndani yako Yesu Kristo Mwokozi wangu nifungue toka dhambi zangu toka dhambi zangu toka mawazo mabaya na ya uharibifu toka maneno yaumizayo na toka kushindwa kufanya leo hasa nakuomba unifungue toka.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

**MAMBO YA KUFANYA KILA SIKU**

Tunaishi katika ulimwengu ambapo kila mtu anabeba udhaqifu uliojaa dhambi na hafia watu wote wanaotuzunguka wanakufa nawasikie maneno "umefunguliwa" nataka kusaidia (Taja majina ya watu hapa

______________________________________
______________________________________
______________________________________

Lete mizigo ya utumwa wao udhaifu wao wa dhambi chini ya msalaba kwa imani na tegemeo waache hatia ilijaa mioyoni mwao wakisikia maneno ya Yesu "UMEFUNGULIWA"
Mambo mengine Bwana ni haya yanayonipa uzito moyoni mwangu leo.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**GUSWA**

**NENO**

Akaweka mikono yake juu yake naye akanyoka mara hiyo (Luka 13:13)
Chukua muda mfupi na fikiri kitu gani kimetokea.

- Mstari 10-11 mwanamke aliyepooza anamsikiliza Yesu akifundisha.
- Mstari 12a Yesu anamwita mwanamke mbele
- Mstari 12b Yesu anamponya mwanamke toka udhaifu wake kwa maneno "Mwanamke umefunguliwa"

Katika mstari wetu wa leo tumekumbushwa kuwa Yesu anahusika na mwili na roho. Utumwa wa mwanamke kwa miaka mingi ulimpooza mwili wake ulikuwa mlemavu.

Mfano ufananao na madhara ya adhabu ya mwili waweza kuwa ni utumwa wa mwili wakati mwingine ukateswa katika utumwa wa vita. Wanaume wamebanwa kwa majuma hata kwa miezi na miaka katika matundu madogo kuliko ukubwa wao. Misuli ya mgongo yao haiwezi kunyooka, wafungwa hukatazwa kusimama wima wanapofunguliwa wanaweza kubaki na sura hiyo ya kuharibika.

**WASWALI KUHUSU HABARI**

1. Katika macho ya fahamu zako ingia katika sinagogi umesikia Yesu anaema "mwanamke umefunguliwa kitu gani kinachofuata (Yesu) anaenda kufanya? Unaomwa akiinuka na kwa upendo anaweka mikono akiinuka na kwa upendo anaweka mikono yake juu yake Rejea zingatia na kibiblia zinatuambia kwamba mara kwa mara Yesu anawagusa watu anapowaponya kwa mfano angalia Luka 4:40.

2. Yesu alimgusa mwanamke mara moja mimi kilitokea hii ina maana gani kwake kimwili? Tabibu mtakatifu amemgusa mwanamke mwokozi wake na Mponya wake aliweka mikono yake juu yake! Sasa utumwa wa mwili wake pia ulivunjwa sasa alifunguliwa moyoni na mwili kutembea alinyooka juu.

**MASWALI YA KUITAFAKARI**

1. Maeneo yapi ya maisha yangu yanaonyesha kweli nimefungwa na ninaishi chini ya mzigo wa dhambi? Ni sehemu zipi za maisha yangu zinahitaji Yesu aguse kwa mikono yake ya uponyaji?

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Katika kuzoea? | Katika ratiba yangu?

Katika vipoumbele vyangu | Katika mawazo yangu?

Katika uwakili wangu? | Katika bitu unavyojali?

Kati8ka mahusiano? | Katika ________________________

2. Orodha yangu ni ipi?  Nini hasa ungependa Yesu akuguse katika maisha yako?
3. Fikiri jinsi gani ungejisikia kuguswa na Yesu na kufunguliwa mwili na roho?

**WAKATI WA KUJIHOJI**

Haya ni mawazo na hisia zinazokuja katika ufahamu ninapofikiri nyakati zile nilipoguswa na Yesu…

___________________________________________________________

___________________________________________________________

___________________________________________________________

Pale alipoweka mikono yake juu yangu…

___________________________________________________________

___________________________________________________________

___________________________________________________________

Haya ni mawazo na hisia zilizokuja katika mfahamu ninapofikiri watu ambao wamekuwa Yesu kwangu –wakinishika au wakinipa wakati wa mguso wa kuniinua na kunisaidia kunitia moyo na kunituliza

___________________________________________________________

___________________________________________________________

___________________________________________________________

**WAKATI WA SALA**

Oh mponyaji mtakatifu Yesu weka mikono yako juu yangu na uniponye.  Yafanye macho yangu kuona na moyo wangu kuisikia neema yako iokoayo.  Mimi ni mwanao aliyeokolewa nitie ujasiri kuangalia kwa uaminifu madhara ya utumwa wa dhambi na kuangalia yale mambo ya hatari


©2008 FULLVALUE MINISTRIES

ambayo nimeyafanya, vilevile kama watu na uzoefu wangu walivyonifanyia. Niguse Bwana Yesu. Niguse katika maeneo ya maisha yangu yaliyojeruhika…

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**MAMBO YAKUFANYA KILA SIKU**

Siwezi kujiponya mwenyewe kuliko mwanamke aliyepooza anaweza kujiponya mwenyewe. Neno la Mungu linatuambia katika mstari wa 11 Kwamba "naye amepindana hawezi kujinyoosha kabisa" sisis sote hatujiwezi temepindana mpaka tutakapoungana na Yesu na kupokea mguso wake wa uponyaji Mungu hutumia watu kuleta upendo wake kwa watu waliovunjika anakutumia wewe na mimi.

Hizi ni jia ninmazoweza kuwa chombo cha upendo wa Mungu kugusa maisha ya wengine.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Leo hasa nafikiri juu ya wale ambao nimekuwa nikiwaombea. Yesu nisaidie mwezi huu kugusa maisha ya watu hawa kwa njia zifuatazo…

1. ____________________________________________________________
2. ____________________________________________________________
3. ____________________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**TUKUZWA**

**NENO**

Akamtukuza Mungu (Luka 13:13b) itikiso la haraka la mwanamke aliyeponywa lilikuwa kumtukuza Mungu. Kitu gani kimetokea kusababisha itikio hilo.

- Mstari wa 12a: Yesu alimwita
- Mstari wa 12: Yesu alimsamehe
- Mstari wa 13: Yesu alimgusa
- Mstari wa 13: Yesu alimponya

Mwanamke aliyepooza ambaye ameona wito wa Yesu msamaha wake, mguso wake wa uponyaji sasa anasimamam kumfukuza Yeyey! Hakuna kinachozuia jinsi ya kumtukuza. Hakuna kinachosimama katika njia yake. Uhusiano wake na Mungu umerudi tena Yuko huru kwa yote yaliyomponya kupooza. Dhambi zake zimesamehewa. Mzigo wake wa hatia umeinuliwa. Historia yake sio kipimo tena cha Hali yake mbele za Mungu na wanadamu Yesu amemponya katika yote ushindi ni wake [Mwanamke] kwa sababu ya jinsi [Yesu} alivyo. Yeye ni Bwana wa vyote!

**MASWALI NA MAONI KUHUSU HABARI**.

1. Neno limesema “akamtukuza Mungu” chimbuka ndani kidogo na soma 1 Timotheo 2:3-5 Fikiri ukweli wa mistari hii. Msitari hii inakuambia nini kuhusu yule aliyemponya nwanamke aliyepooza, kuhusu yule aliyemtukuza?

    - Mungu anapenda watu wote waokolewe
    - Mungu anataka wote wapate elimu ya ukweli
    - Kuna Mungu mmoja.
    - Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu.
    - Mpatanishi huyu ni Yesu ambaye alijitoa mwenyewe kama kafara kwa ajili ya Wokovu wetu.

2. Katika kitabu chote cha Zaburi, watu wa Mungu wametiwa Moyo kumsifu Bwana katika mistari ifuatavyo zingatia misisitizo iliyotumika kutuambia kumsifu Bwana na orodhesha baadhi ya mambo ambayo tumetiwa moyo kumsifu yeye [Bwana].

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Kwa mfano, katika Zaburi ya 100:1-3, Mungu anatuita sisi kushangilia, kumtukuza na kuja mbele zake, kwani twajua ya kwamba ndiye aliyetuumba.  Sisi tu wake, tu watu wake, Kondoo wake

Andika Mawazo yako kuhusu Zaburi hizi:

1. Zaburi 103:1-5
2. Zaburi 146:1-2, 6b-10
3. Zaburi 18:3

**MASWALI YA KUJIHOJI**

Ninapogundua kwamba maisha yangu kama mtoto wa Mungu ni kumtukuza, kuna tofauti gani itatokea? …

1. Kwa jinsi ninavyolinganisha familia na marafiki?
2. Jinsi ninavyofikiri mtazamo wangu kwa kazi yangu wajibu wangu?
3. Kwa jinsi ninavyotathmini historia yangu na kutafuta maono mapya kwa maisha yangu yajayo?
4. Jinsi ninavyojitahidi kuwafikia wale ambao hawana tumaini?

**WAKATI WA KUJIHOJI**

Tumia maswali ya kujihoji kama mwongozo wa kufikiri mawazo yanayofikirika toka fikra mpya na za ndani katika kuelewa na kukuza maisha ya kutukuza [Ibada].

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**WAKATI WA SALA**.

Tumiza orodha ya mambo yaliyopatikana katika Zaburi iliyopita kumtukuza Mungu jinsi unavyomfikiri kwa yote yal e aliyotenda.

Oh, Bwana, Moyo wangu umejaa sifa jinsi ninavyoangalia yote ulivyo na yote uliyoyafanya na unayoendelea kunifanyia. Leo nataka kuanza kukusifu wewe kwa ajili ya ____________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**MAMBO YA KUFANYA KILA SIKU**.

Naangalia vinavyonizunguka naona miti. Inainua matawi yao juu kumsifu muumba wao. Nasikia ndege nasikitiza wanavyoimba nyimbo zao za sifa kwa muumba wao. Naona milima imesimama imara kama sanamu zenye nguvu inayotukuza jina la Bwana.

Lakini namwangalia jirani yangu mlango unaofuata anayeishi gizani, ambaye amepooza naye hajuihilo. Nawaona wafanyakazi wenzangu wanaoishi maisha ya kupooza na wanaona hakuna sababu ya kumtambua yeye aliyewaumba, yeye anayewapenda na kuwasamehe. Rafiki zangu waonekana kufikiri wanakila kitu na kumbe hawana chochote. Hatia inawatumikia kukosa upendo kinawatia makovu na mambo ya kiroho yanawakera.

Watu hawa ni mzigo moyoni mwangu sasa. Oh Yesu tumia maisha yangu ya kukutukuza kugusa maisha kwa ajili yako siku hizi zijazo. Fanya urafiki, kimbilio salama kwa mut huyu ili niweze kusema naye jinsi ulivyobadili masiha yangu na ulivyoniinua kwenye maisha ya kusifu na kufukuza.

Leo, Bwana, nisaidie nitoe ushuhuda wa maisha yangu kwa wengine kwa

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

Leo nataka nitoe kimbilio salama, mahali pa huruma ya Mungu kwa

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**ZUIWA**

**NENO**

Basi mkuu wa Sinagogi alikasirika kwa sababu Yesu ameponya mtu siku ya Sabato akajibu, akawaambia mkutano, kuna siku sita zifaazo kufanua kazi, basi njooni mponywe katika siku hizo, wala si katika siku ya Sabato.

Mamabo gani yametendeka katika mstari huu?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**MASWALI NA MAONI KUHUSU HABARI**

1. Yesu anafahamu sheria. Ilikuwa sheria gani katika Kutoka 20:8-10?

   ______________________________________

   ______________________________________

   Mkuu wa Sinagogi pia anafahamu sheria kwa mtazamo wake Yesu alikwua akivunja sheria kwa kuponya siku ya Sabato.

2. Mkuu wa Sinagogi alidhamiria kunyunyiza maji katika sikukuu ya ushindi wa mwanamke katikati ya kucheza kwake [Mwanamke] kwa Kusifu, kiongozi huyu huyu msomi wa sheria, huyu mzalendo wa dini wa jamii aliyeheshimiwa ameamua kukosoa, kulaumu nakufanya mzaha kwa tendo la Yesu. Mwanamke alisimama katikati hadharani. Fikiri mfadhaiko wa wakati ule. Watu waliokuwa wakiangalia wamekuwa sehemu ya aliyetupwa.

   Angalia maandalio yao! Hayana mistari.

3. Yesu ndiye hujibu. Yesu anamuonyesha kiongozi anayejihesabia haki (kwa) huruma yake (Yesu) inadhihirisha mioyo yao ya binafsi. Anawakumbusha kwamba wanafanya kazi siku ya Saboto kwa kupelekea mifugo yao ya shmaba kunywa maji. Thamani ya wanyama wao yapita thamani ya maisha ya binadamu. Sheria na mipaka yake ya fanya na usifanye inachukua nafasi thamani kubwa kwao kuliko neema na rehema za Yesu alizozitoa katika Sabato hii mpya!

**MASWALI YA KUTAFAKARI**.

1. Fikiri wakati umekuwa katikati ya sherehe na mtu mmoja ameloa mvua katikati ya maandamano yako kutatokea nini katika sherehe yako?

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

2. Watu huangalia jinsi tunavyoyapokea maisha wakati jambo Fulani zuri likitokea watu huangalia kuona jinsi gani tutakavyolitunza wakati jambo Fulani baya likitokea watu hushangaa jinsi tutakavyofanya. Wakati mgumu ukija watu huangalia kwa mbali. Tunaposherehekea kuingilia kati kutakatifu kwa Mungu ndani ya maisha yetu mara kwa mara watu huitikia kwa maswali na mashaka.

   Itikio langu ni nini kua jinsi watu walivyopokea?

3. Wazuiaji ni wale waishio wamefungwa na vizuizi na hatari zao wenyewe wanasisitiza kwambe wengine waishi kama wao. Bila kujua wao huishi wamepooza na wenye mizigo, mashaka wasiwasi na woga wa kukataliwa umewasukuma kulazimisha hali ya kutokuwa salama kwa wengine. Wameangukia kutafuta sababu sio kufanya jambo la maana na wanakazana katika kusongasonga fibra zao kwa wengine ili kujaribia kuthibitisha na kuwabana. Wazuiaji wanabana mpango endelevu. Hawawezi kupokea mabadiliko. Wanakataa kila kitu na kila mtu anayefikiri au kufanya tofauti na wao wanaishi kwa kutawaliwa na woga na bilashaka kwa hali yao wenyewe ya kupooza. Wanajitahidi kuwabana wengine waendelee kufungwa kama wao, wakiwazuia wengine kuishi kama watu waliokombolewa. Nami hao wanaokaza kwamba nibaki nimefungwa badala ya kunitia moyo kuishi maisha ya kufunguliwa? Nani au nini kizuizi? Je naweza kuacha matendo ya wanaonizuia kuniathiri? Wakati gani? Jinsi gani?

**WAKATI WA KUJIHOJI**

Mawazo mengi yanakuja kichwani mwangu najua kwamba niliishi maisha kama ya mtu aliyepooza. Lakini pia najua Yesu amesema nami kwa njia ya maneno toka Luka 13. Moyo wangu umefunguka toka mzigo mzito wa hatia Yesu amenigusa kwa mkono wake wa uponyaji ametoa makovu na maumivu niliyoteswa na wengine.

Lakini nitafanyaje iwapo watu Fulani na mambo Fulani hayataniruhusu niishi huru? Yanataka nibaki nimefungwa, yananizuia kusimama nimenyooka juu.

Pata nafasi na fikiri watu na mambo yanayokufanya ubaki umefungwa isipokuwa utegemee uwezo wa Mungu kukutia nbuvu uishi maisha ya ushindi. Fikiri juu ya hatua ya kinga na chaguo litakalo kutunza uishi maisha ya kufunguliwa kuwa huru na msamaha na uponyaji wa Yesu. Kumbuka kuzingatia mambo hayo kama mahusiano magumu, mambo mabaya uliyoyazoa, na ratiba isiyo ya kujitoa. Waeleze watu na mambo yanayokuzuia na mwulize Mungu kwa uponyajio wake.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**WAKATI WA SALA**.

Oh Bwana nimewatambua wale wanaojaribu kuniaminisha woga wao na vizuizi vyao.  Wanataka wanimalize kwa majaribio kwa kunizuia na kubidhibiti lakini umenifungua.  Moyo wangu unawainua kwako.  Wewe ni mwokozi wangu.  Wakati adui zangu wanapokuwa wengi na wenye nguvu tumaini langu pekee ni kwako [Yesu]  Naungana nawe katika sala yako Yesu "Baba, wasamehe kuwa hawajui walitendalo.

**MAMBO YA KUFANYUA KILA SIKU**.

Yesu, Nawatambua wanaozuia maishani mwangu wewe ni asili ya tegemeo langu na kutiwa moyo kwangu.  Umewaleta watu maishani mwangu ambao ni asili ya nguvu.  Asanta kwa wamekuwa zawadi kwangu.  Asante [Yesu] hasa kwa watu wafuatao:

Nimewatambua kuwa wamekuwa Baraka kwangu, Bwana wiki hii natamani kuwa asili ya kutia moyo, nguvu kwa wengine.  Hasa nataka kuwatia moyo.

Watu hawa wote wameishi katika wakati mgumu Bwana Yesu nifanye asili ya kuwatia moyo kwamba waweze kuyatoa maisha yao kwako watie nguvu waishi maisha ya kufunguliwa na kusamehewa.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**THAMINIWA**

**NENO**

Tutaangalia machimbuko matatu.

Katika mstari toka Luka. Yesu anazungumza juu ya mwanamke ambaye amemponya amemthamini na anaongea kuhusu yeye kwa wapinzani wake “na huyu mwanamke, aliye wa uzao wa Ibrahim.”

Huyu ni mwanamke wa kiyahudi, mmojawapo wa wateule wa Mungu mwenyewe.

“…na huyu mwanamke, aliye uzao wa Ibrahim…” (Luka 13:16).

Fungu hili la maneno linalotuongoza kwenye chimbuko la pili toka Isaya maneno haya yamesemwa kwa wana wa Israel. Kwa jinsi mtetezi wake Yesu alivyotaka kuweka wazi maana ya kuwa uzao wa Ibrahim. Anawakumbusha adui zake kwamba mwanamke aliyetheaminiwa na Mungu kama aliyeumbwa naye, amekombolewa, ameitwa kwa jina, ametajwa kuwa wake.

Lakini sasa, hivi ndivyo Bwana asema yeye aliyekuumba …usiogope nimekukomboa, nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu” (Isaya 43:1).

Haikuwa hali yake ya mwili au hisia wala hali ya uzoefui wake wa maisha, mzigo wake wa utumwa au dhambi zake zilizomsukuma [Yesu}. Kilichokuwa cha muhimu kwa Yesu ndicho alichompa, thamani yake ya kukombolewa kama mtoto aliyesamehewa wa Baba wa mbinguni.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengi, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

**MASWALI NA MAONI KUHUSU HABARI**.

Kwa maneno yako, shirikisha wengine kitu gani kilimfanya mwanamke awe mwanamke wa thamani. ________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

Nani au kitu gani kinasababisha thamani ya kitu? Jibu rahisi: Ni yule anayekimiliki! Kama una kitu ninachokihitaji unaamua bei, thamani ya kitu hicho. Kama sithaminishi kitu Fulani kama unavyofanya wewe, sitwaweza kulipa kwa bei hiyo, kwa maana nyingine kama kitu kinathamani kubwa kwangu nitalipa kwa bei ulioiweka hata kama kwa kiwango cha kafara.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Katika Yohana 3:16  Yesu anaonyesha thamani kubwsa uliyonayo kwa Baba.  Mwanaye, binti wa Baba wa mbinguni.  Yesu anataka wewe ufahamu thamani yako ilivyo.  Napenda ujue upendo mkubwa wa Baba kwako Pendo lililomfanya aridhike.  Kumtoa mwanawe mmoja na wa pekee.

Ili kukununua wewe tena na kukufanya Wake.  Jinsi gani una thamani!  Ni hazina gani iliopo.

Kwa maneno yako mwenyewe shirikisha wengine ina mana gani kwako kuwa mtu wa thamani kubwa.________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**MASWALI YA KUTAFAKIRI**.

1. "Tazameni ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu, na ndivyo tulivyo!" (1 Yohana 3:1)  Mungu ananiita mtoto wake!  Jinsi gani kifungu hichi cha maneno kinahusiana na Yesu anapomwambia mwanamke aliyeponywa kama "Mwana wa Ibrahimu."
2. Jinsi gani haya maneno yanaathiri mtazamo ninaona mwenye, mtazamo ninao angalia mali ya thamani, na thamani yangu yote?
3. 1 Yohana 2:1 inasema "watoto wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhmabi na kama mtu akitenda dhambi tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki."  Jinsi gani mistari hii inakusaidia kurudisha ufahamu wako wa thamani, achilia mbali mambo mengine mabaya unavyojisikia.  Achilia mbali maisha yaliofifia na yenye makovu.

Tofauti gani inatokea kwako kwamba Yesu ni mwenye haki wako kwamba Yesu mwenye Haki ndiyo mtetezi wako?

Hapa ni furushi la thamani ya Mungu kwa ajili yako "sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.  Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhmabi na mauti" (Warumi 8:1-2).

**WAKATI WA KUJIHOJI**.

Kufikiri kwamba Yesu ni mtetezi wangu katika uwanja wa maisha inanikumbusha tena kwamba nina thamani kubwa kwake [Yesu]  Fikiri hasa katika nyakati Fulani maishani unapojisikia peke yako ukipambana na maisha na kutaka kuwa mwenye kukumbuka kwamba Yesu ni mtetezi wako.

Leo nakuhitaji Yesu kama mtetezi kwa sababu.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

**WAKATI WA SALA**

Bwana Yesu, unaniambia jinsi upendo ulivyo "Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake."

(Yohana 15:13) Umetoa maisha yako kwa ajili yangu umenifanya rafiki yako. Umenifanya mali yako ya thamani. Ni zaidi ninavyoweza kutambua ninasimama katika kicho cha upendo katika neema yako na huruma zako umenipa haki yote na nafasi kama mtoto wa mfalme Mungu aliye juu sana. Mawazo yangu yabubujike kwa shukrani. Nashukuru kwa kuchukua yote yaliyoniaibisha na kunichakaza katika maisha yangu na kunirudishia thamani kamili kupitia maisha yako, kifo na kufufuka. Oh Yesu Moyo wangu unabubujika kwa shukrani na sifa. Asante kwa…

**MAMBO YA KUFANYA KILA SIKU**.

Sasa najifananisha na sarafu ya thamani iliyookotwa mtaani. Nimekuwa nikipigwa, burutwa na kupoteza mng'ao. Lakini Yesu ameniokoa nina thamani kubwa kupitia kwake. Yeye ni mgao inikingayo, zaidi kama ganda litunzalo sarafu ya thamani katika mkufu wangu wa funguo Zaburi 3:3 inanikumbusha kwamba Mungu ni "ngao yangu pande zote." Yeye ni mwenye utukufu anayetawaza utukufu wake juu yangu na yeye ndiye "ananiinua juu kichwa changu" Wakati baba akiniangalia kupitia Yesu ananiona Mwenye thamani ya juu kwake. Nani maishani mwangu katika wiki hii anayehitaji kusikia habari za sarafu ya thamani inayoogofya? Ni bwana gani unayemuwazia kama mtu Fulani ambaye angebarikiwa kuona kwamba wewe pia ni mtu uliyejaa thamani kupitia Yesu?

Nadhamiria kutumia mkufu wangu wa funguo nikiwa na maana ya kushirikiana na wengine habari za Yesu. Andika njia dhahiri utokayotumia mkufu wako wa funguo kupata nafasi kumuunganisha mtu kwa Yesu.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES